**Maswali na Majibu**

1. Neno 'mwanafunzi' linamaana gani?
   *Mtu anayejifunza na kufuata*.
2. Yesu alifanya nini kabla ya kuchagua wanafunzu 12?
   *Aliomba usiku kucha*.
3. Wanafunzi 12 walifanya nini?
   *Walisikiliza Yesu na kumsaidia kwa kazi yake*.
4. Marafiki 4 walifikisha mtu aliyepooza kwa Yesu namna gani?
   *Walimteremshia kwa dari ya nyumba*.
5. Yesu alionyesha viongozi wa dini kwamba ana uwezo wakusamehe dhambi namna gani?
   *Alikuwa na nguvu za Mungu na akaponya aliyepooza*.
6. Yesu alionyesha namna gani uwezo wake kwa hali ya anga?
   *Alituliza dhoruba kubwa*.
7. Yesu alilisha watu wangapi kwa mikate 5 na samaki 2? *Alilisha watu 5,000.*
8. Peana mifano 2 kwa sababu gani Yesu hakutaka watu wamfanye mfalme?
   *Hawakutaka kubadilisha mienendo yao, walitaka chakula tu. Wakati haukuwa umetimia yeye kuwa mfalme.*
9. Yesu alifufua nani kutoka kwa wafu? *Lazaro*
10. Nini inafanyika kwa watu walioamini wakifa?
    *Wanarudi kwa mchanga mpaka Yesu atakapokuja ndiyo awatoe kutoka kwa wafu*.

## Mistari ya kukariri

Yohana 15:10  Marko 4:39  Yohana 11:25

## Mazungumzo

Tunajifunza nini kwa uchaguzi wa Yesu vile alichagua wanafunzi - alifanya nini kabla ya kuchagua, aina ya watu aliowachagua, vile alikaa na Yuda? Tunaweza kuwa wanafunzi wa Yesu namna gani?

## Kuandika

Andika vile Yesu alifufua binti wa mjane wa Naini. (Luka 11 – 18) AU binti wa Yairo (Luka 8:40 – 56)

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 32 Kazi ya Yesu

**SOMA Marko 1:16 – 19; Marko 2:1 – 14; Luka 6:12 – 16; Marko 4:35 – 41; Marko 6:32 – 44;**

**SOMO**

Yesu alikuwa na kazi nyingi ya kufanya. Alikuwa afundishe watu juu ya Ufalme wa Mungu na vile Mungu anataka watu waishi. Yesu alitakiwa awe na wasaidizi. Alichagua watu 12 ili wamsaidie kwa kazi ya kufundisha watu. Hawa watu 12 waliitwa wanafunzi, yaani watu wakusoma na kufuata. Wanafunzi walisoma kutoka kwa Yesu. Walipomaliza kusoma, walianza kusaidia Yesu kufundisha na kuita wengine wamfuate Yesu. Yesu alitakiwa kuchagua watu wazuri na waaminifu ili wamsaide. Aliomba Mungu usiku kucha ili Mungu amsaidie awe na uchaguzi mzuri. Siku iliyofuata alichagua wanafunzi 12.

Hawa wanafunzi walikuwa watu wa kawaida na kazi zao za kawaida. Petro, Andrea, Yakobo na Yohana walikuwa wavuvi. Yesu alipowaita, waliacha nyavu zao na kumfuata. Petro, Yakobo na Yohana walikuwa marafiki sana wa Yesu, na baada ya kifo cha Yesu walifanya kazi nyingi sana ya kuhubiri Injili. Mathayo alikuwa mtoza ushuru. Watoza ushuru walichukiwa na Wayahudi kwa sababu walikusanyia Warumi pesa. Filipo labda alikuwa Myunani. Simoni alikuwa mwanasiasa wandani. Yesu anaita watu wa aina yote kuwa wanafunzi wake. Yesu hana haja na kazi zetu au kama sisi ni watu wa maana. Yesu ana haja na msimamo wetu na anataka tumuudumie Mungu.



*Mathayo - Mtoza ushuru*

Yuda Iskariote alikuwa mmoja wa wanafunzi. Baadaye alimsaliti Yesu. Yesu alijua kwamba Yuda atamsaliti, lakini alimchukuwa kama wanafunzi wengine wote. Alikubali Yuda kulinda mfuko wa pesa wa wanafunzi hata kama alijua yeye si mwaminifu.

Wanafunzi waliacha kazi zao na wakasafiri, wakizunguka na Yesu kwa karibu miaka mitatu. Walimsikiliza Yesu na kumsaidia kwa kazi yake. Mungu alimpa Yesu nguvu ya uwezo wake. Yesu alitumia hizi nguvu kufanya miujiza mingi. Miujizi hizi zilionyesha watu kwamba Yesu ni Masiya. Zilionyesha kwamba mafundisho ya Yesu inatoka kwa Mungu.

Yesu alitumia hizo nguvu za Mungu kuponya watu wengi. Hiyo kuponya watu ilionyesha vile Yesu alipenda na kujali watu. Yesu kila mara alisaidia watu waliokuwa na haja. Aliponya viwete, vipofu, viziwi na bubu. Aliponya wenye ukoma, waliokuwa na kifafa na wazimu.

Siku moja Yesu alikuwa amekaa kwa nyumba na viongozi wa maana wa dini. Umati wa watu ulizingira hiyo nyumba. Walitaka kumsikiliza Yesu. Walitaka Yesu atibu wagonjwa wao. Pia kulikuwa na watu wanne waliokuja kuona Yesu. Walikuwa na mgonjwa wao aliyekuwa amelala kitandani. Walijaribu wafike kwa mlango wa nyumba. Lakini kulikuwa na watu wengi zaidi, na ikawa vigumu kupenya kwa umati wa watu.

Wale watu wanne walitumia ngazi ya nje ya nyumba kupanda kwa dari ya nyumba. Walitengeneza shimo kubwa kwa dari ya hiyo nyumba ili watelemshe yule mgonjwa mpaka kwa nyumba ndani. Yule mtu alikuwa amepooza. Hangeweza kujisongesha. Yesu alimwangalia na kumwambia kwamba umesamehewa dhambi zako. Waliokuwa kwa nyumba walishangaa na kusema, “Ni Mungu tu, anaweza kusameha dhambi. Yesu aliwambia kwamba atawaonyesha uwezo wake wa kusameha dhambi. Alimwambia yule aliyepooza, “Simama. Chukua godoro lako na utembee.” Papo hapo yule mtu alipona. Alisimama na kutembea.



Yesu alionyesha viongozi wa dini na watu wote kwamba alikuwa na nguvu za Mungu. Yesu alikuwa na uwezo wa kusameha dhambi. Alikuwa na uwezo wa kuponya watu. Yesu alikuwa Masiya, Mwana wa Mungu.

Pia Yesu alikuwa na nguvu za Mungu na ana amri juu ya anga. Siku moja Yesu alikuwa na wanafunzi wake kwa mashua kwa Bahari ya Galilaya. Kukatokea dhoruba ya upepo wa nguvu na mashua ilikuwa kwa hatari ya kuzama. Yesu aliambia dhoruba, “Nyamaza, utulie.” Upepo na mvua zikaisha. Hiyo dhoruba kuu ikapotea na bahari ikatulia. Yesu akaokoa wanafunzi kutoka kwa dhoruba.

Siku moja umati wa watu ulifuata Yesu mpaka mahali tambarare ili wasikilize mafundisho yake. Ilipofika jioni, Yesu aliona watu wamechoka na walikuwa na njaa. Yesu aliuliza wanafunzi wake walete chakula. Walileta kijana mmoja aliyekuwa na mikate mitano na samaki wawili. Yesu alichukua hizo mikate na samaki. Aliomba Mungu na akashukuru kwa hicho chakula. Akamega hiyo mikate na samaki halafu akawapa wanafunzi ili wapee wale watu wote. Kulikuwa na watu zaidi ya elfu tano na chakula kilitosha watu wote. Hatimae chakula kilichobaki, wanafunzi waliokota vikapu kumi na mbili.

Huu muujiza ulifurahisha kila mtu. Watu walitaka kumfanya Yesu awe mfalme. Yesu hakutaka yafanyike hivyo. Alijua watu hawakukuwa tayari kubadilisha njia zoa na wafuate mafundisho yake. Walitaka mfalme wakuwapea tu chakula. Haikukuwa wakati wa yeye kuwa mfalme kwa hivyo alitoka kati yao ili wasimfanye mfalme.

Pia Yesu alikuwa na uwezo wa kufufua wafu. Alifufua mtoto wa mwanamke mjane. Mwana wa huyu mwanamke alikuwa anatolewa kwa mji wa Naini kwenda kuzikwa. Alifufua binti wa miaka 12 wa Jairo mkuu wa Sinagogi hapo Kapernaumu.

Lazaro rafiki mkuu wa Yesu aliishi Bethania_pamoja na dada zake, Mariamu na Martha. Lazaro alianza kuwa mgonjwa na dada zake wakatumana Yesu aje. Lakini Yesu hakuja Bethania haraka. Baada ya siku mbili, Yesu aliambia wanafunzi wake, “Lazaro amelala.” Wanafunzi walisema kama Lazaro amelala ni vizuri. Lakini Yesu akawaelezea, “Lazaro amekufa.”

Yesu alipofika Bethania, alikutana na Martha. Martha alimwambia kwamba kama Yesu angefika mapema Lazaro hangekufa. Martha aliamini kwamba Yesu angemponya Lazaro. Martha akaongezea akasema, “Ninajua kwamba Mungu atakupea chochote utauliza.” Yesu alimjibu, “Kakako atakuwa hai tena.” Martha alimwambia, “Ndiyo najua ataamka kwa ufufuo wa mwisho.”

Yesu alijibu, “Mimi ni ufufuo na uzima. Yeyote aniaminiye, ataishi hatakama atakufa…”

Halafu Yesu akaenda kwa kaburi. Kaburi ilikuwa pango na jiwe limefingirishwa kwa mlango. Ilikuwa ni siku nne tangu Lazaro afe, kwa hivyo lazima mwili ulikuwa unanuka. Yesu aliambia watu wafiringishe jiwe, walitoe. Aliita kwa sauti, “Lazaro, kuja inje!” Hakukuja vizuri kwa sababu alikuwa amefungwa kwa nguo za kaburi. Yesu aliambia watu wamtoe hizo nguo na wamwache aende.



Yesu alifundisha kwamba wanaoamini wakifa, ni kama kulala. Wafu hawanafahamu. Hawajui lolote. Hawaendi mbinguni. Wanarudi kwa mchanga chini. Hawana uzima kamwe. Yesu atakaporudi hapa duniani, atafanya waliokuwa na imani kuishi tena. Kifo cha walio na imani ni kama usingizi mrefu, hawana fahamu kule kaburini, mpaka Yesu aje awaamshe.